TANGAZO LA SERIKALI NA. 844 la tarehe 11/10/2024

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8 (1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA YITWIMILA YA MWAKA, 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga eneo la Yitwimila ya mwaka, 2024.

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na ya kina katika eneo lililoainishwa kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya ya Busega.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

“Unaanzia kwenye alama ya mpaka wa upimaji namba MV360 yenye majira - nukta 559803MS, 9729194KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS175$^{0}$12’1”MS kwa umbali wa kilomita 2.35 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV349 yenye majira – nukta 560001MS, 9726846KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS265$^{0}$25’55”MG kwa umbali wa kilomita 5.50 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV347 yenye majira – nukta 554541MS, 9726695KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ345$^{0}$25’55”MG kwa umbali wa kilomita 2.00 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV248 yenye majira – nukta 553994MS, 9728692KZ; baada ya hapo mpaka

*Tangazo la Serikali Na. 844 (Linaendelea)*

unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ23$^0$10’17”MS kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV249 mpaka ulipoanzia.”

Dodoma,
2 Oktoba, 2024

DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*